# TAARIFA FUPI YA HALI YA VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI MKOANI MWANZA

# 24/02/2017

# Utangulizi

- Mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa mikoa ya kanda ya ziwa na una halmashauri za wilaya 8.
- Mkoa una Jumla ya wakaazi **3,250,817**
- Watoto chini ya mwaka mmoja ni **122,537**
- Watoto chini ya miaka mitano ni 586,465.
- Akina mama wenye umri wa kuzaa 15 - 49 ni **743,772**
- Vijana wenye umri wa miaka 10-24 ni **1,047,337**
- Ongezeko la ukuaji wa wakaazi ni 3.2.


# Huduma za afya ya uzazi na mtoto

- Mkoa una Jumla ya vituo **388** vinavyotoa huduma za afya.

- Kati ya vituo hivyo vituo **314** vinatoa huduma jumuishi za afya ya uzazi na mtoto ikiwemo;

  - ✓ Uzazi wa mpango, kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, huduma za saratani ya matiti na kizazi, Huduma za chanjo na huduma kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia.


# KIWANGO CHA MATUMIZI YA UZAZI WA MPANGO




**CHANGAMOTO!**

- ✓ Changamoto kubwa za matumizi ya uzazi wa mpango ni uelewa mdogo wa njia za kisasa za uzazi wa mpango.
- ✓ Upungufu wa ujuzi kwa watumishi.
- ✓ Upungufu wa huduma za uzazi wa mpango karibu na jamii.
- ✓ Imani potofu kwa wanaume kuhusu matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango.

# MAHUDHURIO YA KLINIKI KWA WAJAWAZITO





- Changamoto kubwa ya hudhurio chini ya wiki 12 za umri wa mimba ni:

✓ Upungufu wa vipimo muhimu Mfano *wingi wa damu, protini kwenye mkojo nk*

✓ Uelewa mdogo wa jamii juu ya umuhimu wa kuhudhuria kliniki chini ya wiki 12 za mimba.


# HUDUMA ZA KUJIFUNGUA




Mkoa bado unakabiliwa na changamoto za kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma ikiwemo:-


- Upungufu mkubwa wa watumishi wa afya.
- Miundo mbinu isiyo rafiki kwa kina mama kujifungua.
- Imani potofu kwenye jamii.
- Upungufu wa vituo vya kutolea huduma za afya.
- Upungufu wa vifaa tiba na madawa. Asilimia 22 tu ya zahanati na vituo vya afya zinatoa huduma za msingi na za kina za dharura (EmONC services)

# TAKWIMU ZA VIFO VYA KIMA MAMA – 2010 HADI 2016





- Kwa ujumla vifo vinavyotokana na uzazi viko juu(150).
- Hopitali ya rufaa ya Bugando imechangia kwa 31% ya vifo vyote vya mkoa. Mwanza kati ya hivi 26% vinatoka nje ya mkoa wa Mwanza.


# Sababu kubwa za Vifo vitokanavyo na uzazi



# Visababishi vya vifo kwa kinamama (%)



# Idadi ya vifo vya watoto wachanga siku 0-28 (2010/2016)




Vifo vya watoto wachanga siku 0-28 vimepungua kwa 37% (2010 -2016)
Sababu kubwa za vifo ni kushindwa kupumua 36%; watoto kuzaliwa njiti 15% & uambukizo 10%.

*Ukosefu wa vyumba vya kuhudumia watoto wachanga na vifaa tiba imeendelea kuwa ni changamoto kubwa ya inayochangia vifo vya watoto.*

# MAFANIKIO

1. Ongezeko la njia za kisasa za uzazi wa mpango kwa asilimia 12% (2010)-18% (2016)

2. Kupungua kwa vifo vya watoto wachanga wenye umri wa siku 0-28 asilimia 30.

3. Kuongezeka kwa akinamama waliojifungulia kwenye vituo vya afya kutoka 46% mwaka 2010 hadi kufikia 53% mwaka 2016.

4. Vifo vya wazazi vinaendelea kupungua kutoka vifo (182)2010 – 151 (2016)

5. Wakina mama wajawazito wanaohudhuria kliniki kwa hudhurio la kwanza 98%
6. Kupungua kwa vifo vinavyosababishwa na kuharisha kwa watoto chini ya miaka mitano
7. Kiwango kikubwa cha chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano 92%

8. Mkoa umefanikiwa kuwa na vituo vya afya 4 vinavyotoa huduma ya upasuaji kwa wakina mama wajawazito

# CHANGAMOTO

1. Upungufu/ufinyu wa vyumba vya kutolea huduma za afya ya uzazi na mtoto.
2. Uhaba wa watumishi wa afya.
3. Watumishi wa afya kutokuwa na ujuzi wa kutosha kutoa huduma za afya ya mama na mtoto.
4. Upungufu wa vyumba vya kuhudumia watoto wachanga
5. Upungufu wa vifaa tiba na madawa
6. Wajawazito na watoto kuchelewa kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mara wanapopata matatizo ya kiafya.
7. Huduma sizizoridhisha wakati wa ujauzito

# CHANGAMOTO…..

- Upungufu wa vituo vya huduma za dharura kwa kinamama; Mfano Mkoa una vituo vya afya 4 tu kati ya 45 vinavyotoa huduma za dharura.
- Imani potofu kwa jamii juu ya matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango.
- Tabia ya kinamama wajawazito kuchelewa kuwahi kliniki hususani chini ya wiki 12 za ujauzito.

# Mikakati ya kukabiliana na changamoto

- Kusimamia fedha za RBF ziweze kuchangia katika kukarabati vyumba vya kujifungua na kliniki za wajawazito kwenye vituo 112 pamoja na vyumba vya kuhudumia watoto wachanga.
- Kuboresha huduma za dharura kwa kufanya usimamizi ekekezi mentorship na usimamizi shirikishi kwenye vituo vya kutolea huduma
- Kujenga/kukarabati vyumba vya upasuaji (theathre)7, moja kwa kila halmashauri.
- Kutoa mafunzo ya huduma ya huduma za dharura kwa watumishi 696
- Kufanya uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa njia za kisasa za uzazi wa mpango kupitia vyombo vya habari